**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# MKUTANO WA TATU

## YATOKANAYO NA KIKAO CHA KUMI NA TATU

**5 MEI, 2016**

**MKUTANO WA TATU - YATOKANAYO NA KIKAO CHA KUMI NA TATU**

**TAREHE 5 MEI, 2016**

## I. DUA

Saa 3.00 asubuhi Mhe. Job Y. Ndugai (SPIKA) alisoma Dua na kuliongoza Bunge.

**Makatibu Mezani**

1. Dkt. Thomas D. Kashillilah
2. Ndg. John N. Joel
3. Ndg. Asia Minja
4. Ndg. Ramadhani Abdallah

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani:-

1. Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

2. Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

3. Taarifa ya Kamati ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

4. Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Katiba na Sheria juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

## III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

| | | | |
|---|---|---|---|
| i) | Mhe. Katani Ahmad Katani | - | CUF |
| ii) | Mhe. Joseph George Kakunda | - | CCM |
| iii) | Mhe. Hassan Elias Masala | - | CCM |
| iv) | Mhe. Dkt. Elly Marco Macha | - | CCM |
| v) | Mhe. Abdallah Ally Mtolea | - | CUF |
| vi) | Mhe. Mariam Nassor Kisangi | - | CCM |
| vii) | Mhe. Esther Nicholas Matiko | - | CHADEMA |

## IV. MASWALI YA KAWAIDA

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

Swali Na.105 – Mhe. Rose Cyprian Tweve
Swali la nyongeza: Mhe. Rose Cyprian Tweve

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

Swali Na.106 – Mhe. Felister Aloyce Bura
Swali la nyongeza: i) Mhe. Felister Aloyce Bura
ii) Mhe. George Malima Lubeleje

Swali Na.107 – Mhe. Frank George Mwakajoka [kny. Mhe. David Ernest Silinde]
Swali la nyongeza: Mhe. Frank George Mwakajoka

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:**
Swali Na.108 – Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki [kny. Mhe. Makame Mashaka Foum]
Swali la nyongeza: Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki

Swali Na.109 – Mhe. Juma Kombo Hamad
Swali la nyongeza: Mhe. Juma Kombo Hamad

**MATANGAZO:**

- Wageni wote waliokuwa kwenye *Gallery* walitambulishwa Bungeni.

- Kamati zifuatazo zilitangaziwa kukutana;

  - Kamati ya Sheria Ndogo,
  - Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii.

- Wabunge walitangaziwa msiba wa mtumishi Ndg. Betty Saro kilichotokea Hospitali ya Mkoa wa Dodoma Asubuhi ya lsiku hiyo.

- Wabunge wote wa Mkoa wa Iringa walitangaziwa kuwa na Kikao mchana baada ya kusitisha Bunge.

- Spika alitoa taarifa ya Mkutao wa EALA wa tarehe 29/4/2016 uliofanyika huko Arusha.

- Michezo ya EA imeongezeka kutoka iliyokuwepo awali kama Golf, kuogelea, kuvuta Kamba na Volleyball na michezo hiyo itafanyika Desemba Nchini Kenya – Nairobi. Aliwataka Bunge sport Club kuanza maandalizi.

**Mwongozo wa Spika:**

1. Wabunge wafuatao waliomba Mwongozo:-

   Mhe. Dkt. Elly Marco Macha alitumia Kanuni ya 68 (7) akitaka kujua kwa nini Naibu Waziri wa TAMISEMI alipojibu Swali la asilimia 5 inayotoka Halmashauri kwa ajili ya mikopo hakuzungumzia Walemavu bali Wanawake na Vijana tu jambo ambalo ni la kibaguzi.

   Serikali ilichukua hoja yake kwamba ushuauri utafanyiwa kazi.

2. Mhe. Joseph Osmunnd Mbilinyi alitumia Kanuni ya (68(7) akieleza jana Bunge lilipitisha kwa haraka Bajeti ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ili Wabunge wa CCM waende kwenye mkutano wao na Mhe. Rais na akataka kujua endapo UKAWA nao wakiwa na Mkutano Bunge linaweza kuahirishwa na kwamba hiki kilichofanyika ni Chama kuingilia Bunge.

   Kiti kilitoa maelezo kwamba kwa utamaduni wa Jumuiya ya Madola *Party Caucus* zinatambulika ila UKAWA siyo Chama.

3. Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu alitumia Kanuni ya 68(7) alieleza jana Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi akijibu Swali Na. 103 alitoa majibu yasiyo ya kweli aliposema hakuna haja ya kuifanyia marekebisho Sheria ya Madini ili iendane na Sheria ya Ardhi kwani hazitofautiani, alisisitiza Kanuni ya 97(1) ya Sheria ya Madini haitoi haki ya *resettlement* kama ilivyo kwenye sheria ya Ardhi na kwamba jambo hilo hufanyika kwa hiari tu. Aliitaka Serikali kufanya marekebisho hayo ili kuondoa mkanganyiko huo.

   Serikali ilipokea ushauri huo na kusema jambo hili litaendelea kujadiliwa wakati pia wa bajeti ya Wizara husika.

4. Mhe. Kasuku Samson Bilago alitumia Kanuni ya 68(7) na 46 kwamba Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo alitoa majibu ya kejeli alipokuwa akijibu swali la upungufu wa maji Arusha ambapo iligundulika umeme ndiyo tatizo na kusema Mbunge akalinde wezi wa umeme kwani Wabunge siyo Mgambo au Polisi na alihoji kama Serikali imeshindwa kutoa ulinzi huo.

   Kiti kilisema majibu ya mwongozo huo yatatolewa baadae ili kujua kilichotokea au mazingira yaliyokuwepo wakati huo lakini alisisitiza ulinzi na usalama ni jukumu la Watanzania wote ikiwemo Wabunge.

## V. HOJA ZA SERIKALI

- Waziri wa Katiba na Sheria aliwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

- Makamu Mwenyekiti wa kamati ya Katiba na Sheria Mhe. Najma Murtaza Giga aliwasilisha maoni ya Kamati juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

- Mhe. Tundu Antiphas Mughwai Lissu aliwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka 2016/2017.

Uchangiaji wa jumla ulifuata na wafuatao walichangia:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1) | Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka | - | CCM |
| 2) | Mhe. Ahmed Juma Ngwali | - | CUF |
| 3) | Mhe. Ali Hassan Omar King | - | CCM |
| 4) | Mhe. Wilfred Muganyizi Lwakatare | - | CHADEMA |
| 5) | Mhe. Hafidh Ali Tahir | - | CCM |

**VI. KUSITISHA BUNGE**

Saa 7.20 Bunge lilisitishwa hadi saa 10.00 jioni.

**VII. BUNGE KURUDIA**

Bunge lilirejea saa 10:00 jioni likiongozwa na Mhe. Naibu Spika (Dkt. Tulia Akson) na mjadala wa Makadirio ya Mapato na Matumizi yaliendelea kwa Wabunge wafuatao kuchangia:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 6) | Mhe. Omari Mohamed Kigua | - | CCM |

**MWONGOZO WA SPIKA**

mhe. Mohamed Omary Mchengerwa alitumia Kanuni ya 65(7) akiomba kuelezwa kama ni utaratibu unaoruhusiwa kwa Mhe. Tundu Lissu kutumia maneno makali kwenye taarifa ya Kambi kama Zanzibar inatawaliwa nk. Na kama siyo utaratibu afute maneno hayo kiti kilieleza kutolea majibu baadaye.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 7) | Mhe. Joseph George Kakunda | - | CCM |
| 8) | Mhe. Kiteto Zawadi Konshuma | - | CCM |
| 9) | Mhe. Anna Joram Gidarya | - | CHADEMA |
| 10) | Mhe. Tundu Antiphas Mughwai Lissu | - | CHADEMA |
| 11) | Mhe. Mariam Nassoro Kisangi | - | CCM |
| 12) | Mhe. Almas Athumani Maige | - | CCM |
| 13) | Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa | - | CCM |
| 14) | Mhe. Devotha Mathew Minja | - | CHADEMA |
| 15) | Mhe. Abdallah Ally Mtolea | - | CUF |
| 16) | Mhe. Goodluck Asaph Mlinga | - | CCM |

Wakati mjadala ukiendelea Wabunge wa Upinzani walisimama kupinga alichosema Mhe. Goodluck Asaph Mlinga kwamba ni udhalilishaji wa wanawake alipewa nafasi mnadhimu, Mhe. Tundu Lissu alitumia kanuni ya 64 (1) (f) (g) mzungumzaji ametumia Lugha ya matusi na kuudhi kiti kilisisitiza pande zote kumia Lugha za Bunge.

Mnadhimu wa CCM, Mhe. Jenista Mhagama naye alipewa nafasi alisema pande zote zimetumia Lugha za maudhi hivyo maneno yote ya maudhi ya pande zote zifutwe kiti kilielekeza maneno yote ya pande zote yafutwe.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 17) | Mhe. Augustine Vuma Holle | - | CCM |

Mhe. Tundu Lissu alimtaka muongeaji athibitishe kauli yake kwamba yeye ana faili Mirembe kwani siyo ya kweli kwa vile yeye yupo timamu na ndiyo maana ni Mbunge. Kiti kilitumia Kanuni ya 72 kumtaka Mbunge afute kauli na alifuta lakini alipoendelea kuchangia aliendelea kurudia jambo ambalo lilifanya Wabunge wa Upinzani kuongea bila mpangilio hivyo kiti kiliamua kumtoa nje ya Ukumbi Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara na uchangiaji ulisitishwa.

**Kuhitimisha hoja**

Wafuatao walipata nafasi ya kujibu hoja

1. Mwanasheria Mkuu wa Serikali
2. Waziri wa Katiba na Sheria

**Kamati ya matumizi**

Bunge liliingia katika Kamati ya Matumizi na kupitia Vifungu vya Wizara husika na kuvipitisha kwa utaratibu wa *guillotine.* Kisha Waziri alitoa taarifa ya Kamati na Bunge lilihojiwa na kupitisha Makadirio ya Wizara ya Katiba na Sheria.

## 4. KUAHIRISHA SHUGHULI ZA BUNGE

Saa 2.26 usiku Bunge liliahirishwa hadi tarehe 6/5/2016 siku ya Ijumaa saa 3.00 asubuhi.

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **DKT. T. D. KASHILILAH** |
| **5 MEI, 2015** | **KATIBU WA BUNGE** |